**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

Anuani ya Simu "Ushirika"
Simu: +255 26- 23 22456
Telefax: +255 26- 23 21973
B.Pepe: ushirika@ushirika.go.tz

Tume ya Maendeleo ya Ushirika
Mtaa wa Kuu,
S. L. P 201
**DODOMA.**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na. LA. 93/288/01/42** **15 Agosti, 2019**

Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa,
**TANZANIA BARA.**

Yah: **WARAKA WA MRAJIS NA. 4 WA MWAKA 2019 KUHUSU VIGEZO VYA KUANDIKISHA VYAMA VYA USHIRIKA KWA MAZAO YA KIMKAKATI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Kanuni za mwaka 2015, amepewa mamlaka ya kuandikisha Vyama vya Ushirika vya aina na ngazi mbalimbali. Vyama hivi vimekuwa vikitoa huduma kwa wanachama wake katika ngazi za vijiji, Kata, Wilaya, Mikoa na Kitaifa.

Usajili wa Vyama vya Ushirika umegawanyika katika ngazi mbili; ngazi ya kwanza inahusisha Vyama vya Ushirika vya Msingi ambavyo husajiliwa na Warajis Wasaidizi wa Mikoa yote Tanzania Bara na Mrajis wa Vyama vya Ushirika akiwa msimamizi mkuu wa Vyama vyote vya Ushirika Nchini anabaki na jukumu la kuandikisha Vyama vya Ushirika katika ngazi ya Upili na ngazi zinazoendelea. Aidha, Mrajis huchukua jukumu la kuandikisha Vyama vya Msingi panapojitokeza mazingira yanayompasa afanye hivyo.

Katika utekelezaji wa majukumu hayo, kumejitokeza changamoto ya usajili wa Vyama pasipo kuzingatia uwezo/uhai wa kiuchumi (viability) ambayo kimsingi kama isipodhibitiwa mapema, inaweza kuhatarisha

uhai na uendelevu wa Vyama vingi vya Ushirika nchini. Hali hii imechangiwa na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kuruhusu uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vinavyofanya shughuli zinazofanana zaidi ya kimoja katika eneo moja na hivyo kutoa nafasi ya uwepo wa Vyama vingi (utitiri) vya msingi ambavyo baadhi vinashindwa kumudu gharama za kujiendesha.

Hivyo, kwakuwa hakukuwa na vigezo vya kusajili Vyama hivyo, nikiwa msimamizi Mkuu wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara, nimeona kuna haja ya kuweka vigezo vitakavyozingatiwa na kila mmoja kabla ya usajili wa Vyama vya Ushirika kwa lengo la kuwa na Vyama Imara na endelevu.

## 2.0 LENGO LA WARAKA HUU

Lengo Kuu la Waraka huu ni kutoa maelekezo na ufafanuzi wa namna ya kutatua changamoto zilizojitokeza ili kuimarisha Udhibiti na Usimamizi wa Vyama vya ushirika nchini. Waraka huu unatoa mwongozo wa vigezo vitakavyotumika kuandikisha/na kusajili Vyama vya Ushirika vya msingi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2015.

## 3.0 VIGEZO VYA KUANDIKISHA VYAMA VYA USHIRIKA VYA MSINGI

Ili kuwa na Vyama vya Ushirika vya msingi Imara, Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa katika kutekeleza majukumu yenu pamoja na masuala mengine, kabla ya kuandikisha na kusajili Vyama vya Ushirika hususan AMCOS, mnatakiwa kuzingatia uzalishaji wa kila zao kama ifuatavyo:-

i. Eneo la Chama liwe ndani ya Kijiji kimoja hadi Kata ikiwa kuna uhitaji wa kuanzishwa kwake;

ii. Uzalishaji kwa Vyama vya Ushirika Vya Msingi vya Mazao ya Kimkakati unatakiwa kuwa kama ifuatavyo:-

a. Zao la Korosho: Uzalishaji kuanzia Kilogramu 700,000
b. Zao la Pamba: Uzalishaji kuanzia Kilogramu 500,000
c. Zao la Tumbaku: Uzalishaji kuanzia Kilogramu 200,000
d. Zao la Kakao: Uzalishaji kuanzia Kilogramu 100,000
e. Zao la Miwa: Uzalishaji kuanzia Tani 50
f. Zao la Chai: Uzalishaji kuanzia Kilogramu 100,000
g. Zao la Kahawa: Uzalishaji kuanzia Kilogramu 100,000
h. Zao la Zabibu: Uzalishaji kuanzia Tani 400 za Zabibu

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MATAKWA YA WARAKA HUU

Waraka huu utaanza kutumika kuanza 15.08.2019, ambapo Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa kwa kushirikiana na Maafisa Ushirika katika maeneo yenu mtapaswa kuhakikisha mnazingatia maelekezo yaliytolewa ili kuwa na Vyama Vya Ushirika Imara vitakavyokidhi mahitaji ya Wanachama wao.

Aidha, mkumbuke kwamba kila usajili wa Chama cha Ushirika unapofanywa, kunakuwepo na nakala nne (4) za Vyeti/Hati za Usajili ambapo nakala moja itabaki Chamani, nakala ya pili itabaki ofisi ya Ushirika ya Wilaya, nakala ya tatu itabaki ofisi ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa na nakala ya nne itatakiwa kutunzwa ofisi Mrajis wa Vyama vya Ushirika ikiwa katika “Public File” ikiambatishwa na nyaraka zote za usajili.

## 5.0 HITIMISHO

Utekelezaji wa Waraka huu utaboresha upatikanaji/usajili wa Vyama vya Ushirika vilivyo imara kiuchumi na vinavyokidhi mahitaji ya wanachama wake na matakwa ya Sheria. Aidha, kama wasimamizi wa Vyama hivyo, mnapaswa kuzingatia vigezo muhimu vilivyoainishwa katika Sheria ya Vyama vya Ushirika na Miongozo inayotolewa na Mrajis mara kwa mara ili kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama hivi. Hata hivyo, endapo itatokea wakati wa utekelezaji wa Waraka huu kuwepo kwa Vyama ambavyo havitaweza kukidhi vigezo husika, uwekwe utaratibu wa kuvihamasisha ili viweze kuunganishwa kama Sheria inavyoelekeza.

Nawatakieni utekelezaji mwema.

Tito B. Haule
**KAIMU MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

**Nakala**: Mhe. Japhet Hasunga (Mb),
Waziri wa Kilimo,
Kilimo IV Dodoma,
S.L.P. 2182,
**40487 DODOMA.**

" Katibu Mkuu,
Wizara ya Kilimo,
Kilimo IV Dodoma,
S.L.P. 2182,
**40487 DODOMA.**

" Mkurugenzi Mkuu,
COASCO,
S.L.P. 761,
**DODOMA.**

" Maafisa Ushirika wote,
**TANZANIA BARA** **-** (**Kwa Utekelezaji**)

‣ Kaimu Katibu Mtendaji,
Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC),
S.L.P. 2567,
**DAR ES SALAAM**

‣ Kaimu Katibu Mtendaji,
SCCULT (1992) Ltd,
S.L.P. 20640,
**DAR ES SALAAM**